**KISWAHILI**
**KIDATO CHA TATU**
**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI**
**JULAI/AGOSTI 2025**
**MUDA: SAA 1 ¾**

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. Mwandikie barua mhariri wa gazeti la Mwangaza ukielezea vyanzo vya ajali barabarani.
**Muundo ni wa barua rasmi**
**Mwanafunzi azingatie hatua zote za barua rasmi.**
<u>**Hoja za viyanzo vya ajali**</u>

- **i)** **Ukosefu wa ujuzi – madereva wengine hawajahitimu, hawajahudhuria mafunzo.**
- **ii)** **Magari mabovu/ makuu kuu barabarani**
- **iii)** **Utepotevu wa maafisa wa usalama.**
- **iv)** **Barabara mbovu**
- **v)** **Ufisadi wa maafisa wa trafiki**
- **vi)** **Mapuuza ya madereva na watumiaji wa barabara kwa jumia**
- **vii)** **Uendeshaji wa kasi kupita kiasi**
- viii) **Ukosefu wa alama za barabarani kama vile matuta na mabango**
- ix) **Kuachiliwa kwa mifugo na wanyama wa pori katika maeneo ya barabara**
- x) **Matukio ya kimaumbike kama vile mafuriko na maporomoko ya ardhi husababisha maafa.**

2. Teknolojia ya kisasa ina faida nyingi kuliko hasara. Jadili.
**Mwanafunzi ajadili pande zote mbili, ya faida na ya hasara, kasha atoe msimamo wake.**
<u>**Faida za teknolojia**</u>

- **i)** **Kurahisisha mambo, kama vile kazi**
- **ii)** **Kurahisisha kazi**
- **iii)** **Kufanya dunia kuwa kama kijiji**
- **iv)** **Kuharakisha shughuli kama za kibiashara**
- **v)** **Kuendesha elimu**

**Kuongeza kiwango cha utengenezaji na uzalishaji wa bidhaa kama vile kilimo.**

- **i)** **Uharibifu wa mazingira**
- **ii)** **Kuharibu maadili**
- **iii)** **Kuongeza tatizo la ukosefu wa ajira**
- **iv)** **Kuongeza uzembe hasa miongoni mwa vijana mfano simu tamba na tarakilishi na vipakatirishi**
- **v)** **Athari kwa tabia nchi (hali ya anga)**

**Mwalimu azingatie hoja zozote zingine mwafaka.**

3. Fadhila za punda ni mateke. (Andika insha itakayowasilisha ukweli wa methali hii.)
**Mwanafunzi asimulie kisa kinachooana na maana ya methali, 'Fadhila za punda ni mateke' yenye maana kuwa; ukosefu wa shukrani kwa watu wanaotendewa wema na hulipa wema huo kwa mabaya.**

4. Tunga kisa kinacho malizia kwa maneno haya. "….sikuupa moyo wangu nafsi ya kujutia niliyotenda. Nilikuwa nimeamua kuyajenga maisha yangu upya.
**Mwanafunzi aandike kisa kitakachomalizia kwa dondoo. Insha ionyeshe masimulizi ya mhusika aliyekuwa amepotoka na maisha yake yakaenda mrama. Lakini akaamua kuyabadilisha kwa kuchukua hatua nyingine badala ya kujutia yaliyopita.**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes